

## UGONJWA WA FUNGWE WA MIWA: TISHIO LA MIWA

### HUSABABISHWA NA VIMELEA VYA FANGASI (SPORISORIUM SCITAMINEUM)

- Hutokea kwenye mimea isiyotunzwa vizuri
- Hupunguza tija kati ya 20–100% kutegemea aina ya mbegu na utunzaji
- Upungufu wa mavuno huongezeka kwa kadiri ya mikato ya miwa
- Ugonjwa hongezeka kwa mbegu zisizo na ukinzani



*Dalili za awali za ugonjwa wa Fungwe*

### DALILI ZA UGONJWA

- Mmea hutoa machipukizi membamba
- Kudumaa kwa shina la muwa
- Machipukizi ya nyasi kama vile zisizopandwa
- Kupungua urefu wa pingili
- Hutoa mijeledi yenye unga mweusi



*Hatua za juu za ugonjwa wa Fungwe*



*Kuenea kwa ugonjwa katika miwa kama nyasi*

### MBINU ZA KUDHIBITI UGONJWA

- Panda mbegu zisizo na maambukizi
- Dalili za awali ng'oa shina na acha likauke
- Ng'oa na fukia mashina yaliyoambukizwa
- Tumia mbegu kutoka kitalu 'B'
- Tumia mbegu zenye ukinzani
- Mashamba yenye maambukizi zaidi ya 4% ni lazima yang'olewe

Kwa maelezo zaidi wsiliana na:

Kaimu Meneja, TARI - KIBAHA, S.L.P, 30031, KIBAHA, TANZANIA

Simu: +255-232402017, Nukushi: +255-232402039, Barua pepe: cmkibaha@tari.go.tz